

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SIMU: 025 - 2502260
Fax: 025 - 2500128
MKURUGENZI MTENDAJI:
Barua pepe: ded@mbeyadc.go.tz
info@mbeyadc.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P. 599
MBEYA.

10.12.2018

YAH: TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya anayo furaha ya kutangaza nafasi za Ajira ya Mkataba wa miaka miwili (2) za **Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (Community Health Workers)** kwa Wahitimu wa Mafunzo ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii .

WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII -NAFASI 141

KAZI ZA KUFANYA

- i. Kutoa Elimu ya Afya katika Ngazi ya Jamii.
- ii. Kuhamasisha Wananchi kujiunga na Bima ya Afya.
- iii. Kutoa Elimu kuhusu Kujikinga na Magonjwa ya kuambukiza.
- iv. Kufanya kazi nyingine watakazoelekezwa na Mwajiri.

SIFA ZA WAOMBAJI:-

- Kuajiriwa waliohitimu Mafunzo ya Mwaka mmoja Ngazi ya Jamii kutoka katika Vyuho vinavyotambuliwa na Serikali.
- Cheti cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha Nne(IV).
- Wahitimu waliopitia utaratibu wa kujiunga na masomo kupitia Wilaya, Kijiji husika watapewa kipaumbele cha nafasi za kazi

MASHARTI YA JUMLA

1. Barua ya maombi ya kazi iliyoidhinishwa na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji husika, kwamba Mwombaji alichaguliwa kujiunga na masomo kwa kupitia Serikali ya Kijiji na anaomba kazi kupitia kwa Kijiji husika.
2. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

3. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
4. Maombi yote yaambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (*Detailed C.V*), ikionyesha umri, Anuani kamili na Namba ya simu ya kiganjani, pamoja na Anuani/Namba ya kiganjani ya wadhamini wasiopungua wawili (2).
5. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (*Passport size*) na iandikwe jina nyuma.
6. Testimonials”,*Provisional Results*”,*Statement of results*”, hati ya matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA).
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
9. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **14.12.2018 saa 9.30 Alasiri.**
10. Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na yawasilishe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji au yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA.
S.L.P 599,
MBEYA.

IMETOLEWA NA:

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA.

